

HALMASHAURI YA WILAYA YA BUCHOSA



MTIHANI WA KWANZA WA UPIMAJI - FEBRUARI 2025 SAYANSI – DARASA LA NNE

Muda: Saa1:30

Mwaka: 2025

SEHEMU A

1. Jibu maswali katika vipengele (i) – (v) kwa kuchagua herufi ya jibu sahihi kisha iandike katika paradesi ulizopewa.

i. Ni kipi kati ya vifuatavyo siyo tawi la sayansi?

- A. Baiolojia B. Kemia C. Fizikia D. Botani []

ii. Afya bora hujumuisha uimara wa vitu viwili ambavyo ni..... na

- A. Mwili na akili B. Mwili na mifupa
C. Mwili na nywele D. Mikono na miguu []

iii. Chakula chenye virutubisho vyote katika uwiano sahihi kinaitwaje?

- A. Chakula bora B. Chakula cha afya C. Mlo kamili D. Mlo safi []

iv. Ni chakula gani kati ya vifuatavyo kinajenga mwili?

- A. Wali B. Maziwa C. Mkate D. Mahindi []

v. Ni chakula cha aina gani kinahitajika kwa wingi katika mlo wa watoto wadogo?

- A. Wanga B. Vitamini C. Maji D. Protini []

2. Oanisha vipengele katika orodha A na vipengele katika orodha B kwa kuandika herufi ya jibu sahihi.

ORODHA A	ORODHA B
i. Ugonjwa unaotokana na nguo chafu	A. Shinikizo la damu
ii. Huzalishwa na vijidudu vinavyokula masalia ya chakula kwenye meno	B. Madini
iii. Ugonjwa unaosababishwa na kutokufanya mazoezi	C. Kiribatumbo
iv. Tatizo linalotokana na mwili kuwa mkubwa sana	D. Tindikali
v. Kirutubisho kinachorutubisha mifupa	E. Harara

ORODHA A	i.	ii.	iii.	iv.	v.
ORODHA B					

3. Chagua neno sahihi kutoka kwenye jedwali kisha lijaze katika nafasi wazi.

Njano, bluu, kijani, nyekundu, kijani, nyeusi

- i. Ni rangi inayoonesha alama za dharura za usalama.....
- ii. Ni rangi isiyoonesha aina yoyote alama za usalama
- iii. Ni rangi inayoonesha alama za amri za usalama
- iv. Ni rangi inayoonesha alama za kukataza au kuzuia za usalama
- v. Ni rangi inayoonesha alama za tahadhari au onyo za usalama



SEHEMU B

4. Jaza katika nafasi wazi kwa kuandika jibu sahihi.

- i. Kuna aina kuu ngapi za magonjwa?
- ii. Magonjwa yanayoenezwa kutoka kwa mtu mmoja hadi mwingine yanajulikana kama.
.....
- iii. Ni ugonjwa gani husababishwa na vimelea viitwavyo plasmodium?
- iv. Mdudu gani ni maarufu kwa kueneza ugonjwa wa kipindupindu?
- v. Ni ugonjwa gani huambatana na kutokwa na vipete mwili mzima?

SEHEMU C

5. Chunguza kwa makini wanyama wafuatao kisha ujibu maswali



- i. Ni mnyama gani yuko katika kundi la mamalia?.....
- ii. Ni mnyama gani yuko katika kundi la amfibia?.....
- iii. Taja jina la mnyama wa kundi la reptilia.
- iv. Andika kundi la wanyama wenye uti wa mgongo ambalo halipo kwenye picha.
.....
- v. Panzi yuko kwenye kundi gani la wanyama?